




THEME: KIMBIA KUOKOA MAISHA YA WATOTO WACHANGA



WILOLESI FOUNDATION MARATHON 12 JANUARI, 2024

Utangulizi.

Wilolesi Foundation inatarajia kuendesha mbio za hisani zitakazofanyika January 12, 2024 zitakazo julikana kama "Wilolesi Foundation Marathon" ikiwa na lengo la kuchangia ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya wodi ya Watoto wachanga katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa Songea. Kauli mbiu yam bio hizi ni: **"Kimbia kuokoa Maisha ya watoto wachanga"**. Tukio hili litapata ufuatiliaji makini wa wadau mablimbali na hadhira kwa ujumla kupitia vyombo mbalimbali vya Habari kama runinga, redio, mitandao ya kijamii.

LENGO KUU

Kutoa msaada wa vifaa tiba kwaajili ya Watoto wachanga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea.

Malengo Mahsusi

1. Kuhimiza michezo ya kukimbia kwaajili ya kujenga afya mwili na akili.
2. Kusaidia shirika na wadau kufikia malengo huku wakisaidia kukoa Maisha ya Watoto wachanga.
3. Kuongeza kufahamiana na marafiki wapya
4. Kusheherekea siku ya Mapinduzi ya Zanzibar

ENEO LA KUKIMBIA

KM 21: Zitaanza uwanja wa Majimaji kuelekea Bomba mbili kupitia Barabara ya Njombe, kutoka Bombambili kuelekea matarawe kupitia Matarawe kupitia Barabara ya mwembechai kuelekea kituo cha Afya Mji mwema kisha kuelekea Kituo cha polisi cha Lizaboni kupitia Barabara ya Pachanne kisha kuingia Barabara ya Mbambabay- Mtwara kuelekea Uwanja wa ndege kisha kurudi Mjini kupitia Barabara ya Mbambabay-Mtwara mpaka benki ya CRDB kisha kuelekea Uwanja wa Majimaji kupitia njia panda ya Mahenge.

KM 10: Zitaanza uwanja wa Majimaji kuelekea Bomba mbili kupitia Barabara ya Njombe, kutoka Bombambili kuelekea matarawe kupitia Matarawe kupitia Barabara ya mwembechai kuelekea kituo cha Afya Mji mwema kisha kuelekea Kituo cha polisi cha Lizaboni kupitia Barabara ya Pachanne kisha kuingia Barabara ya Mbambabay- Mtwara kuelekea Buhemba kisha kuelekea Uwanja wa Majimaji kupitia Barabara ya Wella.

KM 5: Zitaanza uwanja wa Majimaji kuelekea Bomba mbili kupitia Barabara ya Njombe, kutoka Bombambili kuelekea matarawe kupitia Barabara ya Matarawe kisha kurudi Uwanja wa Majimaji kupitia Barabara ya Manzese.

Namna ya Kushiriki:

Mbio hizi za hisani zitakua katika makundi matatu ambayo ni Kilomita 21, 10 na Kilomita 5. Ambapo kiingilio ili uweze kushiriki mbio hizi ni Tsh. 35,000/= kwa Kilomita 21, Tsh. 30,000/= kwa kilomita 10 na Tsh. 25,000/= kwa Kilomita 5, bei hizi zitajumuisha usajili na fulana kwa ajili ya mbio ambazo zitagawiwa siku chache kabla ya mbio hizo. Kwa wadau ambao hawatashiriki mbio lakini watapenda kuchangia mbio hizi tunawakaribisha kuchangia kiasi chochote.

Washindi wa mbio hizi watatunukiwa zawadi kama ifuatavyo:

Kwa Kilomita 21

1. Mshindi wa kwanza atazawadiwa Tsh.500,000 na medali
2. Mshindi wa pili atazawadiwa Tsh. 300,000 na medali
3. Mshindi wa tatu atazawadiwa 150,000 na medali

Kwa Kilomita 10

1. Mshindi wa kwanza atazawadiwa Tsh.250,000 na medali
2. Mshindi wa pili atazawadiwa Tsh. 150,000 na medali
3. Mshindi wa tatu atazawadiwa 75,000 na medali

Kwa Kilomita 5

1. Mshindi wa kwanza atazawadiwa Tsh.150,000 na medali
2. Mshindi wa pili atazawadiwa Tsh. 100,000 na medali
3. Mshindi wa tatu atazawadiwa 50,000 na medali

Appendix 3: Wadhamini, wafanyabiashara na wadau

Wadhamini (makampuni, wafanyabiashara, taasisi na watu binafsi) wanaotaka kushiriki au kudhamini mbio hizi watachangia kama ifuatavyo:

1. Mchango wa 500,000 na zaidi atapata dakika 5 za kutangaza biashara au huduma kwenye sherehe za ufunguzi na kufunga pia kuweka matangazo wakati wote wa matukio
2. Mchango wa 300,000 hadi 499,999 atapata dakika 2 za kutangaza biashara au huduma kwenye sherehe za ufunguzi na kufunga pia kuweka matangazo wakati wote wa matukio
3. Mchango wa 150,000 hadi 399,999 atapata fursa ya kuweka matangazo ya picha kwenye matukio.

NB: Malipo yafanyike kupitia akaunti namba **023172000141** Jina la Akaunti ni **WILOLESI FOUNDATION, JINA LA BENKI NBC**

